**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

# TAASISI YA UTAFITI WA MISITU TANZANIA

*Utafiti wa Misitu na Ufugaji Nyuki kwa Maendeleo ya Uchumi wa Viwanda*



## 1. UTANGULIZI

Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge la Tanzania Na. 5 ya mwaka 1980. Majukumu ya Taasisi hii kufanya utafiti wa misitu, kuratibu, kutoa na kusambaza matokeo ya utafiti kwa wadau kwa ajili ya maendeleo endelevu ya misitu na viwanda vya misitu nchini. Aidha mwanzoni mwa mwaka 2019, Taasisi iliongezewa majukumu mengine ya kufanya na kuratibu utafiti wa ufugaji nyuki na kusambaza matokeo ya utafiti kwa wadau.

Makao makuu ya TTaasisi yapo Morogoro na ina ofisi katika vituo saba vya utafiti ambavyo vipo Dodoma, Kibaha, Malya, Moshi, Mufindi, Tabora na Lushoto.

## 2. MUUNDO WA TAASISI

Taasisi ina Bodi ya Wakurugenzi ambayo ndio inasimamia shughuli zote za utafiti, na inakutana kila baada ya miezi mitatu. Vile vile kuna Mkurugenzi Mkuu ambaye ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za Taasisi.

Tatu: 1. Kurugenzi ya Utafiti wa Uzalishaji Misitu; ambayo ina sehemu tano ambazo hushughulikia utafiti katika nyanja zifuatazo: utunzaji na uendelezaji wa misitu ya asili, misitu ya jamii na kilimo misitu, uboreshaji wa miti ya kupandwa, upimaji wa mazao ya misitu iliyopo nchini, sera, uchumi-jamii na usambazaji wa teknolojia na matokeo ya utafiti kwa wadau. 2. Kurugenzi ya Utafiti wa Matumizi ya Misitu; ambayo inashughulika na utafiti katika nyanja za: kemia mbao, muundo mbao, uhandisi mbao, kazi msitu na matumizi yake, nishati mbao, uchumi jamii na masoko ya mazao yatokanayo na misitu. 3. Kurugenzi ya Utafiti wa Ufugaji Nyuki yenye sehemu mbili amabazo ni Mazao ya Nyuki na Huduma na Usimamizi wa Makundi ya Nyuki na Manzaki, ambayo utafiti: juu ya ufugaji nyuki na uhifadhi wa nyuki; na 4 Kurugenzi ya Fedha na Utawala, ambayo hujihusisha na masuala ya fedha, uhasibu, utawala na rasilimali watu. Pia Taassi ina vitengo vinne ambavyo ni Manunuzi na Ugavi, Ukaguzi wa Ndani, Tehama na Huduma za Sheria.
Vituo vya Utafiti vinaongozwa na Wakurugenzi wa Vituo, ambao huwajibika moja kwa moja kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi kwa maswala yote ya kiutawala na utafiti.

## 3. KAZI ZA TAASISI

- ◊ Kuanzisha majaribio kuhusu upandaji miti, ukuaji, hifadhi, na matumizi ya miti ya asili na ya kigeni.
- ◊ Kunzisha na kusimamia manzuki.
- ◊ Kuchunguza magonjwa na wadudu waharibifu wa miti na nyuki na njia za kuyazuia.
- ◊ Kuratibu tafiti za misitu na ufugaji nyuki na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa serikali, asasi mbalimbali na wadau wengine juu ya matumizi ya teknolojia bora/mpya ya miti/misitu, hifadhi ya udongo, mimea nyuki na zana za ufugaji nyuki.
- ◊ Kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya uanzishaji, na uendelezaji wa viwanda vya mazao ya misitu na nyuki.
- ◊ Kushirikiana na serikali na mdau ye yote katika utoaji wa vifaa kwa ajili ya kufundisha watafiti.
- ◊ Kukusanya na kusambaza matokeo ya utafiti kwa wadau.
- ◊ Kuhamasisha uhifadhi wa misitu na hifadhi za nyuki, kutoa ushauri wa kitaalamu, na kuongeza uzalishaji, uuzaji, utumiaji wa mazao ya misitu na nyuki

Kazi hizo hapo juu zimeainishwa katika Mpango wa Utafiti wa Misitu wa Taifa (*National Forestry Research Master Plan II*) 2011 – 2020 na Mpango Mkuu wa Kwanza wa Taifa wa Utafiti wa Nyuki (2020 – 2030). Nakala zake zinapatikana kwa kutuma maombi kwa Mkurugenzi Mkuu.

## 4. MIPANGO YA UTAFITI

Kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, sera na mazingira, chapisho la Kwanza la Mpango wa Utafiti wa Misitu wa Taifa (*National Forestry Research Master Plan - NAFORM*) 2000 – 2009 lilihaririwa upya likiwashirikisha wadau mbali mbali na kutoa Mpango wa Pili wa Utafiti wa Misitu wa Taifa (*NAFORM II*) 2011-2020 na Mpango Mkuu wa Kwanza wa Taifa wa Utafiti wa Ufugaji Nyuki. Mipango hii inatekelezwa na Mpango Mkakati wa Taasisi (*Corporate Strategic Plan*) wa mwaka 2021 hadi 2026.

Mpango Mkakati una vipaumbele sita vya utafiti kama ifuatavyo:

1. Utunzaji na uendelezaji wa misitu ya asili
2. Misitu ya jamii na misitu shamba
3. Misitu ya kupandwa na uboreshaji wa miti
4. Ukadiriaji wa mazao ya misitu
5. Uchumi – jamii, sera na ugani
6. Kazi msitu na matumizi ya misitu

### 4.1 Utunzaji, Usimamizi na Uendelezaji wa Misitu ya Asili

Mpango huu unalenga katika kuboresha utunzaji, usimamizi na uendelezaji wa misitu kwa kutumia mifumo mbalimbali ya uhifadhi wa misitu ya asili ya Tanzania. Kuna aina nne za mifumo ya ikologia, nayo ni: misitu ya milimani, misitu ya miombo, misitu ya mikoko, na misitu kingomto.

### 4.2 Misitu ya Jamii na Misitu Shamba

Mpango huu unalenga katika kuhifadhi mali asili ya taifa na mazingira kwa ujumla, pamoja

na kuchangia katika uzalishaji endelevu wa chakula, malisho ya mifugo na kuni kwa wananchi wa vijijini na kando kando ya miji. Pia mpango huu unalenga katika kuchunguza aina mbalimbali za ikolojia ambazo zinachangia katika uzalishaji endelevu wa chakula na mazao mengine ya miti, na utafiti juu ya matumizi ya miti ya asili iliyopo mashambani.

### 4.3 Misitu ya Kupandwa na Uboreshaji Miti

Mpango huu una lengo la kutoa teknolojia za kuhakikisha kuwepo kwa uzalishaji endelevu katika misitu ya kupandwa ya asili na kigeni kwa ajili ya matumizi. Mpango pia unalenga katika kuendeleza afya bora ya miti iliyopandwa.

### 4.4 Ukadiriaji wa Mazao ya Misitu

Mpango huu unalenga kuongeza uwezo wa taifa kukusanya, kutunza na kusambaza habari na takwimu kamili na sahihi juu ya miti na misitu kwa ajili ya matumizi ya taifa na kimataifa.

### 4.5 Uchumi-Jamii, Sera na Ugani

Unalenga katika kuboresha sera ya misitu na uamuzi bora katika kuanzisha, umilikaji na uhifadhi wa mazao ya misitu kwa ajili ya maendeleo ya jamii na uchumi wa Tanzania kwa ujumla.

### 4.6 Kazi Msitu na Matumizi ya Misitu

Unalenga kuongeza na kuendeleza uvunaji endelevu wa mbao ambao utaboresha matumizi ya misitu na kupunguza madhara katika mazingira. Pia kuendeleza na kutoa teknolojia ambayo itaongeza utumiaji (nishati, miti na vifaa) mbadala wa miti na misitu kwa lengo la kuhifadhi mazingira.

### 4.7 Uendelezaji Ufugaji Nyuki

Ili kuhakikisha kuwa kuna uhifadhi endelevu wa nyuki na makazi yao na kuongeza uzalishaji wa mazao ya nyuki na huduma, Taasisi inatekeleza vipaumbele sita kama vilivyoanishwa hapachini:

1. Uhifadhi wa nyuki wang'atao na makazi yao;
2. Uhifadhi wa nyuki wasiong'ata na makazi yao;
3. Uvunaji, uchakataji na ufungaji wa mazao ya nyuki;
4. Viwanda na huduma zinazojikita katika ufugaji nyuki;
5. Masoko na mfumo wa uuzaji wa mazao ya nyuki; na
6. Uchumi-jamii, sera na ugani

## 5. MIPANGO SAIDIZI

### Ushauri wa Kitaalamu

TAFORI inatoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja zote zilizotajwa. Hii ni njia mojawapo ya Taasisi kujitafutia kipato kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake katika uendeshaji. Mpaka sasa, Taasisi imeshatoa ushauri wa kitaalamu katika asasi mbalimbali na kwa watu binafsi.

## 6. VITUO VYA UTAFITI

Vituo vya Utafiti vilivyopo ni kama ifuatavyo:

Kituo cha Utafiti wa Upandaji Miti Nyanda Ukame, Dodoma,
S.L.P. 1576,
Dodoma, Tanzania.

Kituo cha Utafiti wa Upandaji Miti sehemu za Pwani, Kibaha,
S.L.P. 30021,
Kibaha, Tanzania.

Kituo cha Utafiti wa Ukuzaji Misitu, Lushoto,
S.L.P. 95,
Lushoto, Tanzania.

Kituo cha Utafiti wa Upandaji Miti Kanda ya Ziwa,
S.L.P. 166,
Malya, Mwanza Tanzania.

Kituo cha Utafiti wa Matumizi ya Mbao, Moshi,
S.L.P. 10,
Moshi, Tanzania.

Kituo cha Utafiti wa Miti Tetefya, Mufindi,
S.L.P. 45,
Mafinga, Tanzania.

Kituo cha Utafiti wa Misitu ya Miombo,
S.L.P. 1960,
Tabora, Tanzania.



Nasari ya Miche TAFORI Makao Makuu



Watafiti wa TAFORI wakiwa katika shughuri za mradi wa ufugaji nyuki

xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx

***Kwa maelezo zaidi kuhusu shughuli za taasisi, tafadhali wasiliana na:***


**Mkurugenzi Mkuu,**

**Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania,**
**S.L.P. 1854, Morogoro, Tanzania.**
**Simu: +255 23 293 5174**
**Nukushi: +255 23 293 5174**
**Barua pepe: tafori@tafori.or.tz**
**Tovuti: www.tafori.or.tz**